


# Sheria ya kudhibiti mikopo midogo itakavyofanya kazi

Alawi Masare, Mwananchi

Taasisi zinazojishughulisha na utoaji wa mikopo midogomidogo nchini zimekuwa zikifanya kazi bila udhibiti mahsusi kutokana na kukosekana kwa chombo maalumu kinachosimamia sekta hiyo.

Taasisi hizo ambazo hutoa huduma za kifedha zinasaidia katika utoaji wa mikopo na hasa maeneo mengi ya vijijini ambako hakuna benki za biashara.

Hata hivyo, taasisi hizo zina matarajio kwamba Serikali iliyopo itayafikiria mapendekezo ya wadau wa sekta hiyo ili kuandaa muswada ambao hatimaye utazalisha sheria iliyokusudiwa.

Chama cha Taasisi za Mikopo Midogomidogo Tanzania (Tamfi) ambacho ni mtandao wa kitaifa wa taasisi zinazotoa huduma hizo wanasema, wamepokea mapendekezo ya Serikali na kuwataka wadau wa sekta hiyo kutoa maoni yao ili kuendelea na hatua nyingine za kuandaa sheria.

"Tulipokea mapendekezo ya Serikali hivi karibuni na tunatarajia sheria itakamilika ndani ya mwaka 2016," alisema Winnie Terry, ofisa mtendaji mkuu wa Tamfi.

"Tumekuwa tukipigania jambo hili la kuwa na usimamizi wa kisheria ili kuifanya sekta hii ikue haraka pia kuwalinda wateja wa huduma hizi. Wakati mwingine inakuwa vigumu kwa taasisi hizi kubadilika na kuwa benki kutokana na mazingira yaliyopo ukizingatia hatuna msimamizi mmoja," aliongeza.

Taasisi hizi za mikopo midogomidogo kama vile Vicoba zimekuwa na mchango muhimu katika utoaji wa huduma za kifedha kwa Watanzania wengi lakini hazina usimamizi maalumu wa kisheria.

Kwa sasa, zinasajiliwa na kupewa leseni zao kwa kupitia sheria mbalimbali ikiwamo Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002; Sheria ya Makampuni (2002); Sheria ya Benki na Taasisi za Kifedha (2003); Sheria ya Ushirika Zanzibar (1986); na Sheria ya Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini.

Hata hivyo, wadau wa sekta hii wanasema sheria hizi hazishughuliki na masuala ya umiliki; uwezo wa kiutawala na usimamizi; ushindani mbovu; upatikanaji wa fedha za mitaji; na uwajibikaji kwa sababu hakuna chombo maalumu cha kuhakikisha utekelezaji wa yote hayo.

Tanzania ina benki 58 lakini ni asilimia 13 ya watu wake wamefungua akaunti wakati asilimia 49 wanatumia huduma za kifedha zinazotolewa na mitandao ya simu.

Licha mapinduzi haya ya kidigitali na utoaji wa huduma za kifedha kwa mtandao, bado mifumo isiyo rasmi ya kifedha inaendelea kuwa na nafasi muhimu ya utoaji wa huduma kwa jamii.

### Sheria inahitajika

Baada ya kufanya utafiti wa kina kuhusu changamoto zinazoikabili sekta ya utoaji mikopo midogomidogo, Tamfi iliandaa muswada ambao iliuwasilisha serikalini kwa ajili ya hatua zingine.

Winnie anasema Tamfi kama sauti ya taasisi zitoazo mikopo midogomidogo itaendelea na ajenda yake ya kutaka uboreshaji wa mazingira ya kisheria ili kuhakikisha mazingira ya kibiashara ya sekta hiyo yanakuwa mazuri na hatimaye kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa Watanzania.

"Kutokuwapo kwa sheria kunakwamisha ukuaji wa sekta yetu hii pia kunamfanya mtumiaji wa huduma asiwe na ulinzi wa kisheria. Nani anasimamia utendaji wa mashirika ambayo baadhi yao wakati mwingine yanafanya kazi bila kuzingatia weledi?" anasema Winnie.

Kupanda daraja kwa taasisi hizi za mikopo midogo na kuwa benki, nayo imekuwa ni kazi ngumu na inayochukua muda mrefu.

**FINCA ni mojawapo ya taasisi za kutoa mikopo midomidogo ambayo imewekeza kupiga hatua nchini na sasa imeanzisha benki ili kuendelea kuwahudumia wateja wake. Picha ya maktaba**

> **MTAZAMO WA WASOMAJI**
>
> **Ramadhan Zuberi, Moshi**
>
> Tanzania sisi ni matajiri wakubwa sekta ya wanyama, misitu, mbuga za wanyama, bandari na kadhalika. Uchumi wetu sisi Watanzania ukisimamiwa vizuri tutakuwa juu kuliko Kenya. Hata elimu ya msingi hadi chuo kikuu bure inawezekana kabisa tuache utani wa kisiasa. Jamani tukae sawa tusonge mbele taifa lina fedha nyingi angalia Raisi Magufuli amekusanya fedha nyingi kwa muda mfupi. Mafisadi wakifilisiwa kwa muda wa miezi sita tu, Wakenya hawatatufikia kiuchumi. Kwanza rais wetu aanze na katiba kwanza ndipo ataweza hayo.
>
> **Abeid Othman**
>
> Tukubali kama nchi hatujadhamira ya dhati ya kutaka kurasimisha biashara za wajasiriamali wadogo. Kwa mfano nini kazi ya ofisi za biashara za wilaya? Kwa nini zisitumike kuwasajili katika ngazi za wilaya? Kwa nini ofisi hizi zisiwe chachu ya kutoa elimu kwa wafanyabiashara ikiwemo urasimishaji? Awamu hii ya hapa kazi tu ianze na maofisa biashara hawa.

"Hii siyo kazi rahisi hata kidogo. Tunatakiwa kufanya vitu vingi sana ambavyo kimsingi huchukua muda kukamilika. Urasimu pia ni mkubwa sana na Bahati mbaya hatuna pa kwenda kukata rufaa maana hatuna mdhibiti maalumu," anasema Winnie.

Kwa msaada wa Taasisi ya BEST Dialogue, Tamfi imekuwa ikishawishi kuboreshwa kwa mazingira ya kisheria na usimamizi wa mashirika ya mikopo midogomidogo.

Pia sasa chama hiki kina matumaini kwamba Serikali mpya iliyopo madarakani italishughulikia suala hili na hatimaye kuwa na sheria.

Winnie anasema, wana matarajio kwamba Serikali itawasaidia kuweka mazingira ambayo yatawawezesha kufahamu wateja wao na hivyo kupunguza uwezekano wa kupata hasara.

Anasema pia ni jambo jema kwa Serikali kuendelea na utoaji wa vitambulisho vya taifa ambavyo ni zana muhimu kwa taasisi za fedha kuwatambua wateja wao.

### Benki Kuu yatoa shaka

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inarahisisha mchakato wa kupandisha madaraja taasisi hizi na kuwa benki.

Ofisa mmoja wa BoT ambaye hakutaka jina lake litajwe anasema benki hiyo inashughulikia jambo hilo kwa kufanya mabadiliko ya baadhi ya kanuni.

"Tulimaliza kutoa msaada wa kiufundi katika kuandaa sheria ya kusimamia taasisi za mikopo midogomidogo na ninachoelewa ni kwamba kuna kanuni zinafanyiwa marekebisho ili kurahisisha mchakato pale taasisi hizi zinapotaka kuwa benki," alisema ofisa huyo.

UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA
BEST-Dialogue
Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo